Jina la Mtahiniwa: ........ Nambari ya Mtahiniwa: ________ /______

1013/2
P1 KISWAHILI
Karatasi 2
P.T.E
Julai/Agosti 2016
Muda: Saa $2\frac{1}{2}$

Sahihi ya Mtahiniwa: ______________

Tarehe: ______________________

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# PRIMARY TEACHER EXAMINATION

KISWAHILI
Karatasi 2

Saa $2\frac{1}{2}$

**MAAGIZO**

*Andika jina lako na namba yako kwenye nafasi ulizoachiwa.*
*Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa.*
*Mtihani huu una sehemu **MBILI** muhimu: **FASIHI** na **MBINU ZA KUFUNDISHIA**.*
*Ni muhimu sana ufuate maagizo uliyopewa mwanzoni mwa kila sehemu.*
*Andika majibu yako kwenye nafasi ulizoachiwa.*
*Usitoe karatasi yoyote katika kijitabu hiki.*
*Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Sehemu | Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|---|
| A | 1 | 15 | |
| | 2 | 15 | |
| | 3 | 15 | |
| | 4 | 15 | |
| | 5 | 15 | |
| | 6 | 15 | |
| B | 7 | 15 | |
| | 8 | 20 | |
| | 9 | 20 | |
| | | **Jumla** | |

**Kijitabu hiki kina kurasa 14 zilizopigwa chapa.**

**Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

© 2016 The Kenya National Examinations Council.

Geuza ukurasa

## SEHEMU YA KWANZA: FASIHI (alama 45)

*Jibu maswali **matatu:** moja la Ushairi, moja la Tamthilia na moja la Riwaya.*

**USHAIRI:** Jibu swali la **kwanza** au la **pili**.

Said A. Mohammed: *Sikate Tamaa.*

1. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yatakayofuatia.*

**Nyoosha Mkono**

Nyoosha mkono, uviringe ngumi, unyanyuwe kwa hasira
Nyoosha mkono, sema hunitumi, ila kwa haki ujira
Nyoosha mkono, alama ya kukataa
Alama ya nguvu

Nyoosha mkono, na macho makali, uwaonyeshe kukerwa
Nyoosha mkono, wataka halali, kwamba hutaki kuporwa
Nyoosha mkono, alama ya kukataa
Alama ya nguvu

Nyoosha mkono, umekula njama, uyakatae madhila
Nyoosha mkono, nyanyua kwa hima, watambue hukulala
Nyoosha mkono, alama ya kukataa
Alama ya nguvu

Nyoosha mkono, jiunge umoja, na wateswaji wenzako
Nyoosha mkono, mwonyeshe miuja, yaondoke masumbuko
Nyoosha mkono, alama ya kukataa
Alama ya nguvu

Nyoosha mkono, ivume sauti, inayojaa kitisho
Nyoosha mkono, mume jizatiti, kwa mangi maamrisho
Nyoosha mkono, alama ya kukataa
Alama ya nguvu

Nyoosha mkono, mumeshikamana, huo ukuta wa chuma
Nyoosha mkono, kitisho hakuna, wao watarudi nyuma
Nyoosha mkono, alama ya kukataa
Alama ya nguvu

(a) Andika ujumbe mkuu unaojitokeza katika shairi hili. (alama 4)

(b) Eleza muundo wa ubeti wa kwanza. (alama 4)

(c) Kwa kutoa mifano, taja mbinu **mbili** za lugha zilizotumiwa. (alama 2)

(d) Bainisha aina **tatu** za uhuru wa kishairi uliotumiwa katika shairi hili. (alama 3)

(e) Andika maana ya: (alama 2)

(i) jizatiti;
(ii) miuja.

2. Kitula King'ei na Amata: *Taaluma ya Ushairi.*

*Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yatakayofuatia.*

**Amina**

Amina umejitenga, kufa umetangulia,
Kama ua umefunga, baada ya kuchanua,
Nakuombea mwanga, peponi kikubaliwa
Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.

Majonzi hayaneneki, kila nikikumbukia,
Nawaza kile na hiki, naona kama ruia,
Mauti sijasadiki, kuwa mwisho wa dunia,
Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.

Nimemaliza kutunga, kwa kukuombeya dua,
Vumbi tena likiunga, roho likirudishiwa,
Mauti yakijitenga, mapenzi yatarejea,
Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.

(S. Robert, *Maisha Yangu Baada ya Miaka Hamsini,* Uk. 5.)

(a) Eleza mambo **matatu** muhimu yaliyotajwa katika ubeti wa mwisho. (alama 3)

(b) Andika ubeti wa **pili** kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(c) Hili ni shairi la arudhi. Thibitisha. (alama 3)

(d) Taja majina **mawili** yanayotumiwa kurejelea mshororo wa mwisho wa shairi hili. (alama 2)

(e) Ni tamathali gani za usemi zilizotumika katika shairi hili? (alama 2)

(f) Andika maana ya 'kuchanua'. (alama 1)

3. **TAMTHILIA**

*Jibu swali la* **tatu** *au la* **nne.**

K. W. Wamitila: *Pango.*

Kulingana na tamthilia ya Pango, maudhui ya taasubi ya kiume yamedhihirika. Fafanua ukweli huu. (alama 15)

4. Kithaka Wa Mberia: *Natala.*

'Palipo na moshi hapakosi moto.'

(a) Eleza muktadha wa maneno hayo. (alama 4)

(b) Eleza uhusiano wa wahusika wanaorejelewa katika dondoo hili.

(alama 2)

(c) Fafanua jinsi ujumbe ulioko kwenye dondoo unavyodhihirika katika tamthilia.

(alama 7)

(d) Taja mbinu **mbili** za lugha zilizotumika katika kauli hii. (alama 2)

**RIWAYA**

*Jibu swali la* **tano** *au la* **sita.**

Lamin H. Omar: *Dunia Mashaka Makuu.*

5. (a) Eleza maana ya sadfa. (alama 1)

(b) Fafanua jinsi mwandishi wa riwaya ya Dunia Mashaka Makuu alivyofanikiwa kutumia mbinu ya sadfa katika kuendeleza maudhui yake. (alama 14)

6. Habwe J.: *Maisha Kitendawili*

"Utokako taabu na wendako ndiko dhikini kwenyewe."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Fafanua sifa **tisa** za mzungumzaji. (alama 9)

(c) Eleza mitazamo **miwili** ya mzungumzaji kuhusu maisha kwa mujibu wa dondoo hili. (alama 2)

## SEHEMU YA PILI: MBINU ZA UFUNDISHAJI (alama 55)

*Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.*

7. Andaa vile utakavyofundisha kipindi cha ufahamu katika darasa la sita. (alama 15)

8. Eleza mambo **kumi** utakayoyazingatia katika ufundishaji wa matumizi ya kamusi katika darasa la tano. (alama 20)

9. Eleza shabaha **kumi** za kufundisha stadi za kusikiliza na kuongea katika darasa la tatu.

(alama 20)